# Gazeti la Kimataifa

## Waabuduo Damu ya Kristo

ASC Mawasiliano ya Kimataifa – Uongozi Mkuu - Via Maria De Mattias, 10 - 00183 Roma

www.adoratrici-asc.org redazioneasc@adoratrici-asc.org


…Kwa Neno Lako…

Lima, Peru 5-28 Luglio 2017

Mwaka XXI – N. 3, Machi 2019


Mhariri





## Maria De Mattias na Mt. Gaspari, kutano lenye kuzaa matunda

Katika kuadhimisha sikukukuu ya mwanzilishi wetu tarehe 4 Februari, kama pia tarehe 4 Machi, tumeongozwa kutafakari zaidi juu ya mang'amuzi ya kiutu na ya kiroho ya Mt. Maria de Mattias na kupyaisha utume wake wa Upendo kwa Mungu na kwa jirani yetu mpendwa.

Kwa kuwa uwepo wake kwetu ni ushirika endelevu na wenye maana, nipenda kumbuka suala hili kukutano kati ya Mt. Maria de Mattias na Padre Gaspari.

Ilikuwa ni Kwaresima ya 1822 na Mt. Gaspari alialikwa kuhubiri huko Vallecorsa. Maria De Mattias, kijana mwenye umri wa miaka kumi na saba, alikuwapo, kati ya umati wa watu, alivutwa, akiwa mwenye hamu ya kujua, mwenye toba, wazi na tayari kukaribisha ishara ya Mungu, ambaye kwake peke yake angeweza kumpa faraja na kuongea naye kuhusu mahangaiko ya moyo aliyokuwa nayo katika miaka hiyo. Mahangaiko yaliyotokana na mateso ya ndani yaliyomsukuma kuelewa maana ya maisha.

Gaspari, mtu wa Mungu, kama vile manabii aliongozwa na hamu moja tu, yaani kwamba mtu wa wakati wake, aliyetishwa na hofu ya dhambi, angeweza kumfunulia joto la upendo wa Mungu kwa binadamu. Hakika, upendo huo ulimgharimu Baba damu yote ya Mwana wake peke.

Maria mwenyewe, anamsimulia Merlini, alipata maono mazuri kwa kumsikiliza Padre Gaspari. Alipokuwa akizungumza, alimwona akionyesha msalaba, na alihisi kwamba maneno yaliyosemwa na mtakatifu yalimhusu yeye. Kwa hiyo, kama tone la maji ambalo linaanguka kwenye udongo mkavu, huulainisha, na mbegu ambayo huanguka kwenye ardhi yenye rutuba, huwa tayari kuota, kwa namna hiyo Maria de Mattias alipata nguvu mpya, ile ya upendo wa Mungu. Alitambua ishara ya muda mrefu aliyotarajia na kujisikia tayari kuufanya huru moyo wake ili kuutolea kwa ajili ya ulimwengu.

Bila shaka katika kukutana huko Maria De Mattias alielewa kile alichotaka, kuwa nani na kwa namna gani. Mang'amuzi ya Mwanzilishi wetu, kama yale ya masimulizi ya Biblia yanatufundisha kuwa kukutana kunaweza kuzaa matunda, ni chanzo muhimu cha kupata majibu sahihi katika maisha yetu, lakini zaidi sana katika mioyo yetu. Kwa hiyo ushuhuda wake unatueleza kuwa imani, utayari, macho huru kutoka hisia potovu, kupokea mambo mpya na tofauti, kujifunua kwa neema, kujiachia kwa uaminifu ili kutupa daima jarife kwa Neno Lake na kuwa tayari kuwa sauti ya Yule anayejifunua kupitia njia za maajabu lakini ambazo daima zipo popote, ni kiini cha kweli cha kukutana.

***Sr. Maria Grazia Boccamazzo,ASC***

## Muhtasari


*Mhariri*
- Maria De Mattias na Mt. Gaspari kutano lenye kuzaa 1

*Nafasi kwa Uongozi Mkuu*
- Shukrani Sr Nadia Coppa 2
- Kutoka Barua ya Sr. Nadia Coppa, Mkuu wa Shirika 4

*Toka Ulimwengu ASC*
- Il Kijiji cha Matumaini 5
- Kuzaliwa kwa Mt. Maria De Mattias, zawadi kwa vizazi vyote 6
- Nyumba ya wasichana Christy - Kolar 7
- Hofu ya uhuru 8

*Nafasi kwa JPIC/VIVAT*
- Mkutano wa VIVAT nchini Hipania 10
- Maria De Mattias huko Katowice 11

*Ndani ya Shirika*
- Kalenda ya Uongozi Mkuu 12
- Siku za Kuzaliwa: tunasherehekea maisha 12
- Waliorudi nyumbani kwa Baba 12

## Shukrani Sr Nadia Coppa

### 4 Februari 2019

Mniruhusu nisalimie! Ni furaha ya kweli kukutana kwa ajili ya kusherehekea pamoja zawadi kuu ya Maria De Mattias. Kila mwaka, natumaini, tunapata mang'amuzi zaidi, ushirika wa kina uliosimikwa na Damu ya Kristo. Damu hiyo ambayo Maria De Mattias alijilisha mwenyewe na ambayo ilimfanya mfuasi, mwabuduo na mtume asiyechoka.

Napenda kuchukua nafasi hii kuwasalimu wote na kuwashukuru kwa dhati kwa sababu mmependa kushiriki tena mwaka huu furaha ya zawadi hii ambayo si tu ni kwa ajili yetu bali kwa ajili ya Kanisa na kwa ajili ya ulimwengu. Tumemsherehekea "mwanamke mwenye nguvu, mfanyakazi asiyechoka, kioo cha fadhila za Kikristo ..."

Tumemsherehekea "mwanamke mwenye vipaji na mwenye akili nyingi, mwenye upendo, mwenye uzuri wa kipekee, mwenye nguvu na mkarimu, mwenye busara na hekima" ... kwa njia ya haya yote yanayoonekana na, lakini yanayoelezwa vizuri, Padre Yohane Merlini anaelezea utu bora wa mwanamke huyu aliyeunganisha kwa namna ya pekee shauku yake kwa ajili ya Mungu na upendo wake kwa ulimwengu. Mwanamke mwenye kushika mambo ya kiroho zaidi ya kimwili.

Tumemsherehekea mwanamke asiye na mkuu, wa kawaida ambaye harudi nyuma katika mambo ambayo yanatakiwa kufanywa zaidi, lakini zaidi mwenye kutoa majibu ya upendo akiishi kwa ajili ya Mungu kwa sababu Mungu alimtaka sana na yeye alitaka kutoa yote kwa ajili Mungu.

Mungu ametubariki kwa zawadi hii, amelibariki Kanisa lake, ameubariki ulimwengu ... ulimwengu wa nyakati zote.

Maono ya kina ambayo yalimfanya Maria De Mattias mtume asiyechoka wa Damu ya Azizi ni yale ya kuwa upendo, na kushiriki katika kujenga upya ushirika ambao Mungu alikuja kuusimika kwa Damu ya Mwana wake. Mpango mzuri wa kuujenga tena ... mpango mzuri wa kushirikiana.

Maria De Mattias alimruhusu Mungu Baba, kwa njia ya zawadi ya Roho wake, kumpa moyo wa Mwana ... moyo uliovunjwa, moyo hai, moyo wenye kuzaa.

Katika mwaka huu wa jubilei ambapo tunakumbuka miaka 185 ya kuanzishwa Shirika, kumsherehekea Maria De Mattias ni tukio zuri sana kwa ajili ya kujisikia wamoja na wenye shauku ileile ya kimisionari.

Hata sisi tunafuata nyayo za ndoto hiyo, na sisi pia, kama Maria, tunataka kufanya kazi kwa nguvu zetu zote, sisi wenyewe, tukitoa kwa msukumo wa kimishonari ile nguvu, ule uhodari uliotiwa alama na Neno la Damu.

Maisha yaliyobadilishwa ya Maria, maisha yaliyofananishwa na yale ya Mpendwa, na ya Uzuri wa Ajabu, kwa furaha ya moyo.

Yeye, kwa kweli, alijua kuunganisha kwa mtiririko mzuri kazi ya kimisionari na tafakari, ili kila siku ajilishe kwa ule uhusiano uliomsukuma kutoka katika ubinafsi. Tunajua kuwa tunaweza kuzaa matunda tu kama tukiwa chini ya Bwana Harusi na kuonja upendo Unaozaa wa Mungu ambaye anajaza na kuneemesha moyo.

Tunataka kumsherehekea Mt. Maria De Mattias, tukikumbuka na kuifanya zaidi na zaidi ndoto yake kujulikane kwa watu, wakati tunapoendelea kuzaa uhai, kila mahali na daima.

Tujisikie kuitwa kuhamasisha tena na kuupa maana tena utume wetu wa ufuasi na wa kimisionari wa walioitwa "kushirikiana na Kristo katika kazi ya ukombozi" (CdV) na wanaotiwa moyo "kukumbatia wakati ujao kwa matumaini" (Papa Francis).

Mara nyingi tunasema kukumbatia wakati ujao. Labda hatujui kile ambacho tunasema. Kwa sababu, kukumbatia ni ishara ya upendo ... kukumbatia ni ishara ya uhusiano ... kukumbatia ni ishara ya usawa ... kukumbatia ni ishara ya uwazi .. kukumbatia ni ishara ya mapokezi.

Kwa hiyo, kama tunapaswa kukumbatia wakati ujao, kukumbatia kunakuwa mfano wa mahubiri yetu.

Kwa ajili ya ulimwengu huu Mungu anataka wanaume na wanawake wenye uwezo wa kukumbatia ..., wenye uwezo wa kukaribia, wenye uwezo wa wema ... wenye uwezo wa kurithisha kwa kila mtu tunu kuu ya heshima ya kiutu. Kwa sababu hakuna asiyeonekana mbele ya Mungu, kwa sababu hakuna anayetengwa kwenye moyo wa Mungu.



# Nafasi kwa Uongozi Mkuu

Hivyo, masista wapendwa, ndugu wapendwa, tujisikie kuitwa kukumbatia ulimwengu, kwa kweli, kwa mikono ya Maria De Mattias, kwa mikono mirefu, wazi, yenye kulinda... Tujisikie kuitwa kukumbatia huu ulimwengu, tukipanda furaha, tukipanda tumaini, tukipanda alama za kiutu.

Kama tunasema kuwa thamani ya mtu ni muhimu, tuifanye ionekane. Kama tunasema kila mtu ni thamani ya Damu ya Kristo, tuchafue mikono kwa ajili ya hali hizi. Ndivyo alivyofanya Mt. Maria De Mattias, bila kuchoka ... kwa ajili ya mpendwa jirani.

Kukumbatia kwa hiyo, ni kufanya maumivu ya wengine kuwa yetu. Bila kuwa na hofu ya kuyaweka ndani yetu, hata kama yanatuumiza. Kujishughulisha ili kupambana, ili kuyaondoa yale maumivu, ili kuyakomboa.

Maria De Mattias aliufanya moyo wake kuwa mahali pa kusikiliza, mahali pa nafasi ya ndani ambako kulikuwa na nafasi kwa ajili ya wote, pale ambapo wote walijisikia nyumbani.

Hivyo turudishe tena hii habari, tuweke nafasi kwa ajili ya wengine, kama alivyofanya Maria De Mattias.

Kwenye lango la kuingia Acuto, kuna sanamu nzuri sana, yenye maana sana: Maria De Mattias yuko nje ili kutengeneza nafsi kwa ajili ya wengine, kwa sababu ameachilia yote.

Tumwombe Bwana neema hii, ili kuweka nafasi kwa ajili ya wengine, lakini kwa kweli, si kwa maneno matupu, kwa sababu tuko vizuri katika kuongea, bali katika uhalisia, katika hali ya kuonekana, bila kutoa samahani nyingi.

Tumeitwa kufanya kama Maria alivyotenda na kuishi, kuwa na hisia, hali ya kuguswa, hamu, mawazo, vionjo, hali ya kuhisi na kuona, shauku aliyokuwa nayo Yesu. Na hili linawezekana kama tunaweka nafasi.

Kwa Maria ilikwepo nafasi yote. Yote kwa ajili ya Mungu! Mungu alimtaka yeye mzima kwa ajili yake na yeye alitaka kuwa wa Mungu bila kijibakiza. Haya ni matashi yetu: kuweka nafasi kwa ajili ya Mungu, kwa sababu ni muhimu hata kama tunaanza, alisema padre Emanuele, ni kuanza tena na tena, lakini inawezekana.

Mniruhusi nitoe shukrani ya pekee kwa Padre Emanuele, Msionari wa Damu Azizi ambaye aliyeongoza Misa hii akiitajirisha kwa tafakari yake na uzoefu wake. Sala ya siku tatu aliyoiandaa kwa ajili yetu na kwa ajili ya jumuiya ambayo inashiriki Misa pamoja ilikuwa yenye utajiri sana na inayoangaza; Aligawa Neno kwa akitukumbusha kwamba utume wetu ni safari ya kuanza daima ... kutoka kwetu wenyewe ... kwa kuteseka na kushiriki ufufuko, tukitamani ukamilifu wa maisha tunayoyaishi kwa utaratibu mzuri ... Upendo mtakatifu.

Tunamshukuru Padre Bill, Mkuu wa Shirika CPPS, Padre Terenzio Pastore na Padre Benedetto kutoka Uongozi wa Provinsi ya CPPS. Tunaungana kwa furaha na kaka zetu –kwa sababu siku ya Jumatano tarehe 6 Februari huko Napoli utaanza mchakato wa kutangazwa kuwa mwenye heri John Merlini. MDM atafurahi huko mbinguni kwa ajili hiyo!

Salamu kwa mapadre waliokuja, na kwa waseminari CPPS kwa huduma ya liturujia. Asante kwanu ninyi nyote kutoka kwenye jumuiya za karibu, kwa kuweza kuungana nasi na shukrani kwa masista wote, waliotawanyika ulimwenguni ambao wameungana na sisi, katika alama ya Damu. Shukrani kwa wazee ambao wanaishi majitoleo magumu ya ugonjwa wao, kwa vijana ambao kwa shauku wameanza safari hii ya kuvutia ya ufuasi. Shukrani kwa masista wanaoishi kwa uaminifu taabu ya safari ya kila siku ya kuruhusu mambo yaende.

Urafiki wenu unaendelea kuwa ushirika na uhai kwa wote.

Salamu nyingi za heri kwenu ninyi masista mliofika kwa ajili ya kusherehekea pamoja nasi jubilei hii, kwa washirika wetu, kwa marafiki, kwa walei wanachama wanaofuata karama yetu, na kwa wote ambao kwa kupitia mfano wa Mtakatifu Maria De Mattias wanajishughulisha kwa shauku ya ndani kufuata nyayo za Mwanakondoo.

Tujiachie tusindikizwe na Mtakatifu Maria De Mattias tukiomba msaada wa urafiki wake, ambaye utakatifu wake "unapendeza na kuvutia".


***Sr. Nadia Coppa, ASC***
***Mkuu wa Shirika***







# Kutoka Barua ya Sr Nadia Coppa, Mkuu wa Shirika



*"pale ambapo huwezi kufika kwa kutenda kazi, fika kwa matamanio. Ishi katika amani. (..) Yesu anazaliwa upya ndani ya mioyo yetu, na anatuvutia kwake, nakubariki kikamilifu."*

*(Padre Yohane Merlini)*

Jumatano tarehe 6 Februari 2019 saa 12 huko kwenye nyumba ya Askofu wa Jimbo la Napoli, katika uwepo wa Kardnali Crescenzio Sepe, ilifanyika sherehe kwa ajili ya ufunguzi wa mchakato wa kutangazwa kuwa mwenye heri Mheshimiwa Y. Merlini.

Baada ya muda wa sala ya mwanzo, Sr. Nicla Spezzati, ASC, anayehusika na mchakato, aliwasilisha ombi la mwongozo wa kesi. Kiapo kilifanywa na katiba ya Mahakama ya Kanisa ambayo itakuwa na kazi ya kusikiliza, kwa miezi inayokuja, ushuhuda, yaani unaoweza kuchangia mambo ambayo yatathibitisha muujiza unaoonekana kutokana na maombezi ya Padre Yohane Merlini.

Hatua hii ya kwanza itaendelezwa kwenye jimbo ambapo muujiza ulithibitika na mahali penye sifa ya maelezo, yaani ya kukusanya uhakiki, itafuata kukabidhi maandishi yote ya jimbo kwa Ofisi inayohusika na kesi za watakatifu. Kwa hatua hii ya mwanzo, itafuata hatua ya pili, akipenda Bwana, hadi mwisho wa maamuzi: Mwenye heri na kufuatiwa na kutangazwa mtakatifu.

Ulikuwa ni muda unaogusa, muhimu sana ambapo tulipata mang'amuzi ya Wema wa Mungu. Bwana anaendelea kulibariki Kanisa na Mashirika yetu mawili yaliyotunzwa na Padre Yohane, akitufanya kuonja maombezi ya huyu Mtakatifu wetu mpendwa na mwenye kuheshimika.

Kwenye adhimisho walikuwepo kikundi cha Wamisionari wa Damu Azizi pamoja na Padre William Nordenbrock, Mkuu wa Shirika, Padre Emanuele Lupi, CPPS ambaye ni msaisizi wa mchakato na Padre Terenzio Pastore, Mkuu wa Provinsi.

Sisi, wa Uongozi Mkuu, tuliungana tukiwa wenye shangwe na Waabuduo mbalilmbali waliokuja kutoka kwenye baadhi ya jumuiya za karibu walioshiriki muda huu kwa shukrani na ushiriki.

Tunamshukuru Bwana kwa zawadi hii ya pekee ambayo inatujaza furaha kubwa moyoni. Bwana anaendelea kutupa moyo kuelekea mabadiliko ya uhakika ya moyo, tujiachie tuwashwe kwa Moto wa Roho na kumruhusu Baba atuzawadie Moyo wa mwana.

Tuombeane ili tukio hili lituguse kwa ndani na kutupa hamu ya kupata utakatifu.

Tusali na kuwaalika wengine kusali ili Padre Yohane Merlini atangazwe na Kanisa kama mfano wa utakatifu.

***Sr. Nadia Coppa, ASC***

# II Kijiji cha Matumaini

**Hali ya sasa na utekelezaji**

Kituo hiki kilianza kufanya kazi tangu 2002 na kimepanua shughuli zake zaidi ya lengo la awali na kimekuwa mojawapo ya vituo vya kutoa huduma na matibabu kwa watu zaidi ya 2750 walioathirika na VVU katika Mkoa wa Dodoma na nje ya mkoa huu.


Utunzaji wa watoto wetu ambao wakati huu wapo 153 hutolewa na wanandoa wa familia 12 na zaidi ya kuwepo familia hizi, kuna msaidizi mmoja ambaye kwa kawaida ni muuguzi ambaye husaidia katika kazi mbalimabali na huduma muhimu zinazohitajika kwa watoto. Wanandoa wanajiandikisha kwa hiari kwa ajili ya kazi hii na wanalipwa kiasi kilichopangwa na Taasisi, zaidi ya malipo hayo wanapewa chakula, malazi na matibabu ya magonjwa ya kawaida. Wanandoa wanaweza kufunga mkataba wao na Taasisi wakati wowote wanapoona hawawezi kuendelea. Wafanyakazi wengine wanaajiriwa kulingana na sheria za Wizara ya Kazi.

Sehemu ya kliniki inahudumiwa na madaktari watatu. Mmoja wao hutembelea kila asubuhi nyumba zote ambako watoto wanaishi na kutoa matibabu sahihi kama yanahitajika. Ikiwa mtoto anahitaji uangalizi maalum, anahamishiwa kwenye zahanati iliyopo katika Taasisi ambako anakuwa akihudumiwa kwa njia sahihi zaidi, Ikiwa mtoto anahitaji uchunguzi wa kimaabara, maabara iko katika Taasisi. Manesi wakunga na manesi wahudumu, na wote wanaofanya kazi katika Taasisi kwa wakati huu wapo 21.

Kwa ajili ya elimu ya watoto, shule ya msingi na sekondari zimejengwa. Kwa watoto wadogo kituo cha huduma ya siku kiko ndani Taasisi.

Shule ni mfano wa ushirikiano kati ya watoto wenye afya na wale walioambukizwa; kwa kweli watoto wenye afya na wagonjwa wanahudhuria shule hizo bila ubaguzi. Shule zimesajiliwa na Wizara ya Elimu, ziko wazi kwa ajili kwa watoto wote, lakini zinaendeshwa na Taasisi yenyewe.

Sehemu kubwa ya mradi huu imetekelezwa na wafadhili wa Italia kwa awamu tofauti. Madaktari wengine na wataalamu wa maabara wanaotoka kwenye hospitali ya Italia ya Bambino Gesù, kwa kawaida huja mara mbili kwa mwaka kwa muda wa wiki tatu. Kwa ya ujenzi tumekuwa na makundi tofauti kutoka Italia kama Amici delle Missioni wa Bagnolo Mella au Impruneta Onlus na mengine mengi, huja mara mbili kwa mwaka kwa muda wa wiki nne kwa ajili ya utendaji wa kazi kwenye idara tofauti za taasisi. Matengenezo yote, mabomba na umeme waliyafanya kwa uhuru na wao. Hatimaye tuna makundi madogo au watu binafsi. Wao huja na kukaa pamoja na watoto kwenye zahanati au wanasaidia kwa njia tofauti kulingana na ujuzi wao.


Sr. Maria Rosaria Gargiulo, ASC, Pd. Vicenzo Boselli. CPPS na Wafadhili


Wanafunzi wa Shule ya Msingi Maria De Mattias


Sr. Maria Rosaria Gargiulo, ASC, Pd. Vicenzo Boselli. CPPS, mfadhili na watoto


Sr. Maria Rosaria Gargioulo, ASC na baadhi ya wasishana (wanafunzi) waliolelewa na kukua katika Kijiji cha Matumaini

*Sehemu II – Historia fupi ya Kijiji cha Matumaini iliyotolewa na Sr. Maria Rosaria Garigiulo, ASC, wakati wa Mkutano wa Mwaka wa Region*

# Kuzaliwa kwa Mt. Maria De Mattias, zawadi kwa vizazi vyote



Mnamo tarehe 4 Februari, masista ASC Region ya Tanzania, wanovisi, aspiranti na wanafunzi, waumini na wafanyakazi wetu, na watu wote wanaompenda Mt. Maria De Mattias tulisherehekea siku yake ya kuzaliwa. Kama sisi, watu wengi wanatambua ukuu wa mama yetu unaojidhihirisha kupitia unyenyekevu na utayari wa kupokea mpango wa Mungu na kujitoa sadaka kwa Bwana bila kijibakiza.



Huko Manyoni, sherehe ilitanguliwa na sala ya siku tatu, ambapo tulimshukuru Mungu kwa zawadi ya Mt. Maria De Mattias na kumwomba Mungu neema yake ili tuweze kuendelea kukumbatia na kuifanya karama tuliyokabidhiwa ikue. Wanafunzi wa Shule ya sekondari Amani walihamasisha sherehe. Maria De Mattias ni msimamizi wa shule yao na wanafunzi wanampenda sana. Baadhi yao wanapenda kusoma historia yake na kufahamu maisha yake kwa sababu wanapenda kufuata njia ya utakatifu, baadhi yao wanapenda kujiunga na shirika baada ya kumaliza masomo yao.

Sherehe ilikuwa nzuri sana, Misa ilianza saa kumi na mbili na nusu asubuhi na iliongozwa na Pd. Alex Isengwa, CPPS akiwa na Pd. Thomas Wambura, CPPS na Pd. Dismas Mfungamali, CPPS. Nani angeweza kufikiri kwamba siku ya kuzaliwa ya mtoto huyu ingesheherekewa sehemu nyingi duniani na vizazi vingi? Tunasherehekea siku ya kuzaliwa Mt. Maria De Mattias kwa sababu yeye alitekeleza mpango wa Mungu. Haya ni baadhi ya maneno ambayo Pd. Alex, CPPS aliyasema wakati wa mahuburi. Kwa sababu hiyo, maisha yake amekuwa ni zawadi inayompendeza Mungu na mpendwa jirani, hii ndiyo sababu ya kusherehekea siku yake ya kuzaliwa popote ulimwenguni.

Kwaya ya wanafunzi ambayo ilihamasisha liturjia iliwaalika wote kusherehekea kwa furaha siku ya kuzaliwa mama yetu kwa wimbo:

"Njoni, njoni, njoni, tumshangilie Mama Maria De Mattias, ni mama yetu Mwema, ametukuka mbingu, njoni tumshangilie ni Mama yetu tunampenda" wanafunzi waliimba pamoja nasi kwa furaha na shukrani kwa Bwana kwa ajili ya maisha na wito wa Mt. Maria De Mattias. Hawa ni wasichana ambao leo wanafaidi ndoto ya Mt. Maria De Mattias kwamba "Katika Shirika hili itapatikana misaada yote leo na daima... (Barua ya MDM, 6, Disemba, 1838, toleo la 2005)

Mt. Maria De Mattias, utuombee ili nasi tuweze kuiga mfano wako katika kujitoa kwa Bwana bila kujibakiza.



***Sr. Rosemary Elias Malele, ASC***

# Nyumba ya wasichana Christy – kolar - India

Nyumba ya shirika ya Aradhana, Christy girls Home Kolar, ni malazi kwa ajili ya watu wengi waliodhaifu katika jamii, nyumba ya watoto ambao wazazi wao wameathirika na virusi vya UKIMWI. Mahali hapa tunakabiliana na mahitaji ya kimwili, kisaikolojia, elimu na ya kiroho, kwa kuzingatia ukuaji mzuri wa watoto hawa, ili waweze kusitawi kama watu wenye uwezo zaidi. Tuna watoto 19 ambao wanafundishwa katika madarasa tofauti, wengi wao wanafanya vizuri katika masomo na wana vipaji vya michezo na sanaa.

Mwaka huu wamekuja kujiunga nasi watoto wapya 6, ambao wote walikuja kupitia wadi ya VVU ya hospitali ambako tunawahudumia wagonjwa wenye VVU / UKIMWI, ambapo hupata huduma ya kupata utulivu au kujiandaa kukabiliana na kifo. Watoto hawa wote wamepoteza baba zao walioathirika na ugonjwa huu unaoua.

Kuna watu wengi pia wanaokuja kushinda na watoto na kutupa misaada yao kwa njia mbalimbali, tunawashukuru wote wale ambao wanafungua mioyo yao kwa ukarimu kujiweka wenyewe katika mshikamano na wale walio wahitaji zaidi. Watoto wetu pia wana nafasi nyingi, kama vile Siku ya Watoto, mipango ya mashindano na vyuo vingine na matukio mengine shuleni na kwenye nyumba yetu, pale ambapo wanaweza kuuonyesha vipaji vyao kwenye ubora wa elimu, katika michezo na katika sanaa wakipata matokeo ya juu.









Kitengo chetu HIV/AIDS kinafanya kazi vizuri, hospitali ya wilaya inatupa miundombinu yote muhimu na dawa kwa ajili ya wagonjwa, tuna uwezekano wa kupata ushauri mara kwa mara wa matibabu, vifaa vya kutosha vya madawa, ultrasound, CT, X-RAY, n.k. na wagonjwa wanafurahia matibabu na wanatoa shukrani zao kwa matibabu wanayopokea.

Sisi watatu: Sr. Chinnammal, Sr. Jyothi na mimi tunajishughulisha kutoa huduma yetu isiyo na malipo kwa wahitaji kupitia utaratibu na msaada wa kiuuguzi, utunzaji wa watoto, kazi za kichungaji parokiani na shambani.

***Sr. Beena Thoombalan, ASC***

Eneo la Bara: Ulaya
Region Italia

# Hofu ya uhuru

Ijumaa, Januari 18, 2019, kwenye Nyumba ya Wafungwa ya Rebibbia ilifanyika sherehe ya kukabidhi tuzo ya Shindano la Uandishi iliyotolewa na Sista wetu asiyechoka Emma Zorda, Mwabuduo Damu ya Kristo, ambaye licha ya kazi zingine nyingi ambazo anazifanya, anatoa kwa hiyari huduma kwenye Nyumba ya Wafungwa ya Rebibbia, anatoa msaada na usimamizi kwa watu waliofungwa wakiwashirikisha katika kazi yake ya uandishi, akiwapa uwezekano wa kueleza hisia zao za ndani kabisa na kuwafanya wasikiwe na ulimwengu wa nje. Ni kitabu cha nne kilichowasilishwa na Sr. Emma tangu mwaka 2014 na mada iliyochaguliwa ilikuwa kweli changamoto kwa wafungwa: "HOFU YA UHURU". Nini hutokea mwishoni mwa kifungo? Yapi ni matarajio na hali halisi nje ya Gereza? Kitabu kilichojaa chakula kwa fikra juu ya hisia, juu ya udhaifu wa kibinadamu, juu ya wajibu ambao kila mmoja wetu anao kuhusu wale waliodhaifu zaidi, juu ya huruma ambayo tunahitaji kuionyesha kwa wale ambao walifanya makosa, maandishi yote yaliyomo kwenye kitabu yanaeleza wazi hofu waliyonayo ya kutokuwa tayari kukabiliana na ulimwengu wa nje, kutoweza kujibu mahitaji ya jamii, lakini zaidi ya yote kukutana na hali ya shida na ngumu kwa sababu ya ugumu wa kifedha ambayo haisaidii sana familia na mara nyingi kwa sababu ya ukosefu wa upendo wa kweli na uaminifu. Kwa neno moja, hofu ya wakati ujao. Sr. Emma alitaka kutolea kitabu hiki kwa Dr. Stefano Ricca ambaye alikuwa Mkurugenzi wa Nyumba ya Wafunguwa ya Rebibbia tangu 2009 na mbaye wakati wote alikuwa akisaidia shughuli za utamaduni na sanaa ndani ya Gereza, akielewa uzuri wake kwa kusudi la kutibu. Alikuwepo Cardinal Petrocchi, mtu mwenye kujali utu na utamaduni ambaye tayari alishashiriki kwenye shindano la kwanza la uandishi, alitoa shukrani kwa mwaliko na nafasi ambayo haya matukio yanatupeleka nje ya ukawaida na ya kila kitu ambacho hakitufanyi tuone umuhimu wake katika mzunguko wa maisha, na kukazia tendo la huruma ambapo hii mikutano inawasilisha kwa ajili ya wafungwa na kwa ajili ya wale wanaohusika nao, alisoma aya ambazo zilitutajirisha na kutuimarisha, akitupa uwezekano na nguvu ya kuinjilisha ulimwengu hasa kupitia mateso ya watu walio pembezoni. Kardinali alieleza habari ya uhuru kwa kukazia kwamba uhuru ni hali ya kiakili na siyo ya nje, kwa sababu mtu anaweza kuwa huru ndani akiwa mfungwa au popote, wakati mweingine mtu anaweza kuwa mfungwa hata nje ya gereza. Njia ya uhuru ni wazi kila wakati hivyo kwamba huu uzoefu lazima ufikiwe na idadi kubwa ya wafungwa na kukaribishwa kwa upendo na wale wanaosoma masimulizi yao. Uhuru si kitu cha gharama ndogo na cha kupatikana kwa gharama hafifu, bali ni lengo la safari ya taabu na uvumilivu na huhitaji msaada wa Mungu. Uhuru unaambatana na ukweli, ni ahadi ambayo Yesu anaieleza kwetu: "Mtaujua ukweli na ukweli utawafanya huru".










Pia alikuwepo Monsignor Dario Edoardo Viganò, Mshauri kwenye Idara ya Mawasiliano ya Vatican, ambaye anaongoza utume wa Kichungaji kwa miaka ndani ya Magereza, wenye mpango "Injili ndani", ukiongozwa na mwandishi wa habari wa Vatican Daudi Dionisi. Monsignor Dario Viganò, akiunganisha shukrani ambazo tayari zilishatolewa na Kadinali Petrocchi, alieleza kwa ufupi jinsi hofu ya uhuru ilivyosambaa leo, kuhusu hali wanayoiishi watu.

Alizungumza kuhusu uhuru, kwa kuuhusisha na wajibu na hatari ambayo ipo daima katika chaguzi za kila siku, wajibu ambao lakini unatufanya sisi kuwa watu. Uhuru kwa hili huleta hofu kwa wote, na kwa sababu hiyo mtu lazima afanye uchambuzi endelevu wa chaguzi zake mwenyewe. Lengo ni lile la kufanya uonekane utakatifu ambao upo ndani ya kila mmoja wetu, kwa sababu Mungu ni sehemu yetu. Kipengele kingine muhimu ni msamaha na kujisamehe ili kufikia utulivu wa moyo.

Waandishi wote walipewa zawadi ambazo Sr. Emma alizifunga kwa upendo na kuwakabidhi kila mmoja wao.

Ujumbe ambao wageni wa Nyumba ya Wafungwa wanatupa ni wazi na unaonekana: tusaidieni kisaikolojia na kwa vitu kwa ajili ya kujiingiza tena kwa uhakika katika jamii, ili kuweza kupokelewa na kupendwa. Ni ujumbe huu unaotoa umuhimu wa kazi za uandishi, kwa kueleza tena maisha yao, kwa kuelewa safari yao, kwa kuwasiliana na wengine na kuelewa mahitaji ya yule asiye na sauti ili kuweza kuyatoa nje.

Asante Sr. Emma Zordan na wote ambao wanajitoa ili kutekeleza hizi kazi nzuri, salamu kwa kikundi cha parokia ya Allumiere ambacho kilishiriki mkutano, kilichowasilisha kitabu cha Kafka "LA TANA"

**Prof. Maria Teresa Caccavale**
*Mwalimu mstaafu kwenye gereza la Rebibbia*





# Mkutano wa VIVAT nchini Hispania

VIVAT ya Kimataifa Hispania ni Shirika lisilo la kiserikali lililoundwa na mashirika nane ya kitawa ya kikatoliki na kuidhinishwa kwenye ECOSOC (Consiglio Economico e Sociale/Baraza la Uchumi na Jamii) la Umoja wa Mataifa.

VIVAT inajishughulisha na kazi zake mbili za utume kwenye eneo la utetezi kwenye Umoja wa Mataifa. Utume wa VIVAT unafanywa kwa njia hii:

- Kufanya kazi na watu na makundi ambayo yanateseka kwa aina zote za umasikini, wakijishughulisha kutunza utu wao, heshima yao na uhuru wao.
- Kusitawisha haki za kibinadamu, maendeleo endelevu, maelewano kati ya watu, tamaduni, makundi, dini na imani; kufanya juhudi katika ujenzi wa jumuiya na wa ulimwengu ambao unahimiza hali ya kuwa pamoja na ushirikishwaji wa wote
- Kufanya kazi kwa ajili ya usitawi wa mazingira, ulinzi wa viumbe hai, na uhifadhi wa utajiri wa sayari kwa vizazi vijavyo.

Tangu wakati wa kuanzishwa kwake, mnamo Oktoba 2015, kundi la VIVAT la Kimataifa la Hispania linafanya ukusanyaji na kuchapisha kesi za hatari za HB (Haki za Binadamu) za wahamiaji na wakimbizi. Dhamira yetu ni kuleta kesi hizi kwa Uchunguzi makini wa Sheria ya wote ya Umoja wa Mataifa ambayo, kwa upande wa Hispania, imepangwa Oktoba 2019.

Huu ni muhtasari wa ripoti hii:




**1.** Hii ni ripoti ya pamoja iliyowasilishwa katika muhula wa 3° Ciclo wa EPU ya Hiapania. Ripoti hii inatoa taarifa juu ya hali ya haki za kibinadamu za wahamiaji nchini Hispania, inajitokeza kwa kufanyiwa kazi na kikundi cha Kazi cha EPU katika kikao chake cha 35 Januari/ Februari 2010. Haki ya binadamu inahusu N ° 9 ya Azimio la pamoja la Haki za Binadamu: Hakuna mtu anayeweza kufungwa kiholela, kufukuzwa au kufungiwa mipaka.

**2.** Ripoti hii iliwasilishwa na Kamati ya Haki na Amani ya Hispania Chama Karibú, Chama cha watu waliounganа, Wahamiaji na Haki (Caritas, Haki na Amani, na CONFER) na VIVAT ya kimataifa..




**mapendekezo:**

- Kumaliza utendaji wa kurudi "kwenye ubaridi" ambao hausaidii haki za wahamiaji kadiri ya sheria za kimataifa.
- Kuwahakikishia misaada na habari muhimu kuhusu uwezekano wa kuomba ulinzi wa kimataifa wahamiaji wasiofuata sheria.
- Kupendekeza kama njia mbadala kambi ya kizuizi ya wahamiaji wasiofuata sheria kwa ajili ya makazi ya muda kwenye maeneo wazi ya mapokezi ya kibinadamu kwa muda unaohitajika ili kuandaa nyaraka

Ninamaliza kwa kukumbuka mawaidha ya Papa Francis kwa Bunge la Ulaya: "Ulaya itaweza kukabiliana na shida za kijamii za uhamiaji ikiwa inaweza kuonyesha wazi utambulisho wake wa utamaduni na kutekeleza kwa vitendo sheria za usawa ambazo zinaendana na ulinzi wa haki za wananchi wa Ulaya ikihakikisha, wakati huo huo mapokezi ya wahamiaji".

***Sr. Teresa Martínez, ASC***

# Maria De Mattias huko Katowice

Wakati nilipokuwa nashughulika na mada pana na yenye kujenga kama ile ya mkutano, sikuweza kufanya chochote zaidi ya kukumbuka siku ya tarehe 4 Oktoba. Siku ambayo, katika mapokeo ya Kikristo, inafanana na mfano wa ajabu wa Mtakatifu Francis, msimamizi wa Italia na ishara halisi ya yeye ambaye, katika kukutana na roho za Viumbe, aliwapa mwanga, kupitia mkono wa Bwana na kurekebisha njia ya kufanya catechesi. Kwa hiyo, haikuwa bahati mbaya kwamba siku hiyo hiyo ya mwaka 2018 Mji wa Vatican ulifanya matembezi ya kikundi cha mahujaji kwenda Katowice, mji wa Polandi ambao ulikaribisha Mkutano wa Umoja wa Mataifa ili kujadili mabadiliko ya hali ya hewa. Mkutano huu ulikusanya nchi 24 toka duniani kote kuanzia tarehe 3 hadi 15 Desemba 2018 kujadili masuala ya mazingira. Matembezi hayo, ambayo yalianza Roma, yaliandaliwa na Shirika la Kikatoliki la Kimataifa linaloongozwa na mtaalam wa mazingira wa Kifilipini Yeb Sano, ili kuleta sauti ya ulimwengu wa Kikatoliki kwa mwaliko wa barua ya Papa Francis "Laudato Sii". Aliyewakilisha Shirika letu ni Sr. Dani Brought, mshauri kutoka Uongozi Mkuu, ambaye aliungana na kikundi cha mahujaji.

Magazeti mengi yaliandika juu ya umuhimu wa tukio hili, ikiwa ni pamoja na gazeti la Yesu ambalo, katika makala yenye kichwa "Mahujaji wa Mzingira", linasema: *"Mkutano usiotarajiwa pamoja Yeb Saño huko Roma pia umemfanya aingie katika safari Sr Dani Brought, wa Waabuduo wa Damu ya Kristo (picha ya mwanzilishi wao, Mtakatifut Maria De Mattias, iliyotolewa kwa Yeb, sasa inasindikiza mahujaji kuelekea Katowice): Miaka ishirini na mitatu ya Utume huko Guatemala ilinionyesha jinsi uchafuzi wa mazingira unavyoathiri sana afya ya watu. Mimi mwenyewe niliishi katika kikundi cha harakati cha upinzani kisichotumia nguvu ambacho kilipelea shughuli za mgodi wa dhahabu kusimama unaoendeshawa na kampuni ya kimataifa. Kila moja ya chaguzi zetu ina athari kwa wengine na hii inajenga ushirika kati ya watu. "*(Yesu n.12 Desemba 2018 p.33)

Tunalishukuru kundi la Global Movement la Kikatoliki ambalo lilikuwa msemaji wa mawazo ya Kikatoliki ili kuzuia matatizo ya mazingira na Sr Dani Brought, ambaye alituwezesha sisi kuwa pamoja na Mt. Maria De Mattias, akiongozana na kundi hilo hadi Katowice. Kwa hiyo "Anza kufanya kile kinachohitajika, halafu kile kinachowezekana na mara utashangaa kufanya jambo lisilowezekana", Mtakatifu Francis wa Assisi.

***Sr. Maria Grazia Boccamazzo, ASC***







## Kalenda ya Uongozi Mkuu




Sr. Nadia Coppa, Sr. Bridget Pulickakunnel,  na Sr. Manuela Nocco watashiriki:
**1 Machi** Mkutano wa Marafiki wa Kijiji cha - Impruneta
**2 Machi** mkutano na kikunci cha Mradi Tanzania cha Bagnolo Mella (Brescia).
**4 Machi** ufunguzi 185° mwaka wa kuanzishwa Shirika
Kuanzia tarehe **15 Machi** hadi **12 Aprili** Uongozi Mkuu utakuwa kwenye ziara katika Region ya Zagreb

## Siku za Kuzaliwa: Tunasherehekea maisha

| | | |
|---|---|---|
| miaka 30 | | |
| **Sr. Kristen Forgotch** | 25/03/1989 | USA |
| miaka 40 | | |
| **Sr. Manuela Nocco** | 06/03/1979 | Italia |
| miaka 50 | | |
| **Sr. Ewa Kleps** | 03/03/1969 | Wrocław |
| **Sr. Palmina Totaro** | 30/03/1969 | Italia |
| miaka 60 | | |
| **Sr. Fina Ponce** | 05/03/1959 | USA |
| miaka 70 | | |
| **Sr. Fidelis Basić** | 07/03/1949 | Zagreb |
| **Sr. Jane Gegg** | 23/03/1949 | USA |
| miaka 80 | | |
| **Sr. Ida Meomartino** | 01/03/1939 | Italia |
| **Sr. Ancilla Vukoja** | 15/03/1939 | Zagreb |





## Waliorudi nyumbani kwa Baba

| | | |
|---|---|---|
| 02/02/2019 | **Sr. Emma Bevilacqua** | Italia |
| 09/02/2019 | **Sr. Elena Palese** | Italia |





**Habiri ya kila mwezi**

*na*
***Waabuduo Damu ya Kristo***
***Mawasiliano ya Kimataifa - Uongozi Mkuu***
Via Maria De Mattias, 10 - 00183 ROMA

**Mwaka XXI, N. 3, Machi 2019**

*Kamati ya wahariri*
**Maria Grazia Boccamazzo, ASC**
**Mimma Scalera, ASC**

Tafsiri na
***Sr. Klementina Barbić*** *- Kikroeshia*
***Sr. Betty Adams*** *- Kiingereza*
***Sr. Martina Marco*** *- Kiswahili*
***Sr. Bozena Hulisz*** *- Kipolishi*
***Sr. Clara Albuquerque*** *- Kireno*
***Sr. Miriam Ortiz*** *- Kihispania*
***Sr. Lisbeth Reichlin*** *- Kijerumani*